REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Thursday, 10th February, 2022

The House met at the Assembly Chambers at 9.00 a.m.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) in the Chair]

PRAYERS

STATEMENT

NOTICE PAPER

Hon. Daniel Nyausi: Thank you, Mr. Speaker. Here are tentative businesses for next week. It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Tuesday (Afternoon) February 15th, 2022.

A. PAPERS- Report of the Agriculture, Environment and Natural Resource Committee on County Government of Laikipia quarterly reports and financial statements for the period between July 2019 and June 2020 for the department of Water, Environment and Natural Resources.

B. PAPERS- Report of the County Cohesion, Justice and Legal Matters Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of County Public Administration.

C. PAPERS- Report of the Education and ICT Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Education and I CT Committee.

D. NOTICE OF MOTIONS- Report of the Agriculture, Environment and Natural Resource Committee on County Government of Laikipia quarterly reports and financial statements for the period between July 2019 and June 2020 for the department of Water, Environment and Natural Resources.

E. NOTICES OF MOTIONS- Report of the County Cohesion, Justice and Legal Matters Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of County Public Administration.

F. NOTICES OF MOTIONS- Report of the Education and ICT Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Roads and Public Works.

G. MOTIONS- Report of the Transport and Public Works Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Roads and Public Works.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Wednesday (Morning) February 16th, 2022.

A. RESPONSES TO STATEMENTS- Response Statement No 004/2021 by the Health Services Committee raised on 22nd July 2021 by Hon. Joseph Kiguru pertaining to Universal health programme so-called NHIF Subsidy for indigents and vulnerable.

B. MOTIONS- Report of the Agriculture, Environment and Natural Resource Committee on County Government of Laikipia quarterly reports and financial statements for the period between July 2019 and June 2020 for the department of Water, Environment and Natural Resources.

It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Wednesday (Afternoon) February 16th, 2022

A. PAPERS- Report of the Auditor- General on the financial statements of Nanyuki Water and Sewerage Company limited for the year ended 30th June, 2019.

B. PAPERS- Report of the Auditor-General on the financial statements of Laikipia County Bursary fund for the year ended 30th June, 2020.

C. MOTION- Report of the County Cohesion, Justice and Legal Matters Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of County Public Administration.

It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Thursday (Morning) February 17th, 2022.

A. PAPERS- Report of the Labour, Social Welfare and Community Services Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Sports and Social Services.

B. PAPERS- Report of the Finance and County Planning Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Finance, County Planning and Enterprise Development.

C. NOTICES OF MOTIONS- Report of the Labour, Social Welfare and Community Services Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Sports and Social Services.

D. NOTICES OF MOTIONS- Report of the Finance and County Planning Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Finance, County Planning and Enterprise Development.

E. MOTION- Report of the Education and ICT Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th June 2020 for the department of Education and ICT Committee.

Thank you, Hon. Speaker and the Members.

Speaker: Thank you, so much Hon. Deputy Speaker.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTION

STATE OF THE COUNTY

(Resumption of previously held debate on 8th February, 2022 at 2.30 p.m.)

THAT pursuant to the provisions of Standing Order No. 24 (4) the thanks of the Assembly be recorded for the exposition of the public policy contained in the address of the Governor delivered on Tuesday, 8th February, 2022 at 2.30 p.m.

Speaker: Hon. Members, we had started a debate on the same but there are Members who did not get an opportunity to contribute and therefore, today we want to give them an opportunity to do so.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nasimama nikishukuru na kuweza kukaribisha Wajumbe katika hiki kipindi baada ya kufungua kutoka likizo. Sasa tumerudi ili tuweze kuendelea na kazi na kuangalia yale mambo ambayo Gavana alisema. Sasa hivi tumerudi ili tuweze kufanya kazi na wakati huu hatutafanya kama wakati huo mwingine ambapo wengine walienda kusherehekea lakini Wajumbe wengine walibaki wakipata shida hapa. Nadhani leo tumerudi kazi sisi wote bila wengine kukaa nje wakingoja malipo.

Bwana Spika, hili ni jambo ambalo tumeweza kuliangalia na kuona ya kwamba wale ambao tunafikiria wanaweza kutuongoza na kutupeleka hatua nyingine wamekuwa ni wanyama wala watu. Nakumbuka wakati uliopita wakati tulikuwa na bodi ambalo lilikuwa na kina Mheshimiwa Thomi na wengine, hili Bunge angalau lilikuwa linaongozwa vizuri. Kwa wakati huu hawa Wajumbe wamekuwa wakifinyiliwa na pia wafanyikazi wamekuwa wakifinyiliwa kwa sababu hili Bunge limekuwa la watu watatu ama wanne ilhali sisi zote tuko na majukumu na nafasi.

Jambo la mwisho ili niweze kuchangia, tunasikia ya kwamba kuna mpango mwingine ambapo wengine wanataka kutoka waende wakasherehekee na walipwe mapesa lakini wengine wabaki kuumia hapa. Wakati tulipofunga tulielezwa vizuri ya kwamba ni kufunga na kwenda nyumbani lakini wengine walienda Canada na walipotoka pale wakaenda Vietnam halafu wakarudi kwenda Israel na hayo ndiyo mambo ambayo tuliyoyaona.

Nafikiria wewe ukiwa Spika sasa wakati huu mambo yatakuwa tofauti na hautasimama hapo wakati sisi wengine tunaumizwa. Sisi zote ni wafanyikazi na hata yule mfanyikazi ambaye anafagia yuko na haki ama yule ambaye ni mwandishi. Hakuna mtu ambaye yuko na haki kushinda yule mwingine. Kwa hayo machache ni vizuri muelewe ya kwamba hawa Wajumbe na wafanyikazi pia hawajafurahia kwa vile mambo yalivyoendeshwa wakati tulipoenda likizo ambapo wengine walibaki hapa Bungeni wakipora pesa na kujilipa wengine wakibaki kuumia. Hata wafanyikazi wengine kulipa nyumba ni shida.

Bwana Spika, nikiangalia katika hotuba ya Gavana, kuna mambo ya ushuru ambapo Gavana alielezea ya kwamba ushuru umekua lakini wakati umekua tunaona ya kwamba tutakuwa na maendeleo katika Laikipia yetu kwa sababu nia yetu kama viongozi ni kuhakikisha ya kwamba wananchi ambao tunawakilisha wanapata maendeleo ya kutosha na wamepewa zile huduma za kutosha.

Bwana Spika, Gavana alisema ya kwamba aliweza kuokota milioni 2.98 katika nusu ya kwanza ya mwaka na hilo ni jambo ambalo nimeliona na nikaliangalia. Nilipopiga mahesabu yangu kama kiongozi, niliona ya kwamba ukisema nusu ya kwanza umepata milioni 2.8 ambayo ni 36%, basi hiyo ni kumaanisha ya kwamba unapojumlisha hiyo mara nne kwa sababu mwaka huwa na robo nne, basi jawabu la hilo hesabu litakuwa 4% kumaanisha ya kwamba

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

pesa ambazo tutaokota zitazidi. Wakati pesa zinazidi basi hiyo ni kumaanisha ya kwamba yule mwananchi ambaye anayefanya biashara hapa kwa mfano yule ambaye anayeuza mboga na yule mwenye duka katika Laikipia anaumizwa.

Ninasema hivi kwa sababu wananchi wetu wameumia na kuna bodi la ushuru ambalo limekuwa likizunguka na viti. Wao hulala na kuamka wakifikiria vile wataongeza pesa kutoka biashara za watu na hilo ni jambo ambalo linaumiza wananchi. Mimi mwenyewe ninataka kupinga vikali vile tunasikia wananchi wetu wakiongezewa pesa za kulipa leseni. Akiongezewa malipo ya leseni ni kumaanisha ya kwamba ile faida ambayo atakayopata kwenye biashara yake, badala ya kumsaidia kuinua biashara yake huwa inachotwa yote na serikali. Baadaye hiyo serikali hutumia hizo pesa vibaya na mamlaka vibaya na hizo ndizo pesa ambazo tunaona zikitumika kugandamiza Wajumbe ambao wanawakilisha katika hili Bunge. Hizo pesa pia ndizo zinatumika kugandamiza wafanyikazi katika hili Bunge kwa sababu hawapewi haki yao na pesa zao huwa hawapati kwa sababu huwa zinaenda kwa mifuko za watu wachache.

Bwana Spika, wakati tunapookota hizi pesa na kuzitumia vibaya, Mungu mwenyewe ambaye yuko juu atajilipishia yeye mwenyewe. Ataona na ataangalia na wale ambao wanafanya hiyo kazi ninafikiria ya kwamba siku moja watalipia kwa sababu hatuwezi kuwa tunashuhudia wengine wakinyanyaswa na wengine nao wanaenda kutajirika peke yao kana kwamba hii Laikipia ni yao.

Jambo la pili ni kuhusu afya. Afya imekuwa na shida kwa sababu Gavana anasema ya kwamba wameweza kubadilisha jina la hospitali kutoka *Laikipia Hospital* na ikaitwa *Laikipia Health Service*. Lile jambo ambalo Gavana amefanya pamoja na watu wake ambao wanaongoza katika hiyo idara ni tu kupaka hospitali rangi na kupanga viti za hospitali ilihali wananchi ambao wako huko hawapati huduma. Nikisema hivyo ninajua ya kwamba leo wako Mirera wakienda kusema ya kwamba wameweka madawa na vinginevyo.

Juzi nilikuwa huko na kile kitu ambacho niliona ni rangi tu imepakwa na wakaandika Laikipia *Health Services* lakini ukiingia ndani badala ya kupata hizo huduma anapata tu ni viti zimepangwa na rangi ikapakwa na hata daktari hakuna. Hata kama wanaitwa Laikipia *Health Services*, mimi sioni hizo huduma kwa sababu sijasikia wala kuguza hizo huduma ambazo zinafaa kuwa katika hiyo hospitali. Mwananchi wangu pia ambaye ninawakilisha hapa, hata yeye hajasikia wala kupata hizo huduma.

Bwana Spika, sisi kama Bunge tunafaa kuungana na pia kukashifu vile wananchi wetu wanaumia katika hizo hospitali kwa sababu hiyo imekuwa ni shida. Mtu akiwa mgonjwa na aiingie katika ile hospitali yetu ya rufaa ya Nanyuki ama akohoe kidogo, wanasema ya kwamba yuko na korona na kuwekwa kwa chumba kilichotengwa cha korona na kulipishwa mamilioni ya pesa na hivyo ndivyo wananchi wetu wanaumia. Mimi nimeitwa katika harambee nyingi sana ambapo watu hushindwa kulipa pesa na nikiulizia shida ni nini, ninaambiwa ya kwamba alipelekwa kwa ICU ambapo hiyo ICU ni mikebe tupu iliyoko na vitu ambazo hazisaidii wananchi wa kawaida na malipo kubwa ya hospitali.

Mimi ningetaka kumwambia Gavana asije kutumia makaratasi kutuambia maneno ambayo haipo. Mimi nakashifu waziri ambaye husimamia Idara ya Afya kwa sababu ninaona ni kama hata yeye haelewi kazi yake. Ndiyo juzi nilisema ya kwamba anafanya kazi lakini hata mambo ya daktari hajui. Niliuliza itakuwaje wewe unaongoza kikosi cha polisi na unataka kupatia polisi masharti ilhali wewe mwenyewe haujapata hayo mafunzo ya polisi. Unawaambia wafanye *mark time* ilihali wewe anaangalia na kuenda tumbo mbele bila kujua ya kwamba *mark time* inafaa wewe usimame kidete na kuangalia mbele. Kwa hivyo hiyo ndiyo ile shida ambayo tuko nayo katika hii hospitali….

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Catherine Nyawira: Hon. Speaker, I rise on a point of clarification. This House has discussed that issue before raised by the same Member and I remember your ruling Mr. Speaker. You said that this is an administrative post and a Governor's appointment. Therefore, the Member should refrain from trying to make it look like it is only a doctor who should lead a hospital. So Mr. Speaker refer to your ruling in the same issue in this Assembly which you had previously made last term.

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, nashukuru kwa vile nilikuwa naendelea. Nimeshangaa ni hoja lipi la nidhamu na liko katika ukurasa upi kwa sababu hauwezi kusimama kwa hoja la nidhamu na hausemi liko wapi. Labda iwe ni hoja la kupata ufafanuzi.

Speaker: Hon. Ndiritu, the Hon. Member had started by saying it is a point of order then said it is a point of clarification, and the clarification was… Please be seated. The clarification was, you see the department of health must not only be led by a medic, simply because the role of the CECM is an administrative role.

Therefore, even the CECM of Agriculture today can be transferred to the department of Health and lead that department because it is more of an administrative kind of role. To treat and other works, the directors should be the ones who are so much in that line of expertise. I think it is important to be informed and not to bring the same issue again and again because it was ruled by the Speaker. Continue, Hon. Ndiritu.

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, nafikiri hayo ni maoni yangu. Nafikiri sheria ya Bunge inampa kila Mjumbe nafasi ya kutoa maoni yake na fikira zake. Sijamkosoa Spika. Najua Spika alisema ya kwamba unaweza kupelekwa kwenye idara yoyote na kuongoza mahali popote. Nikasema kwenye maoni yangu kuwa leo uko hapa kama Spika na ninajua ulipochaguliwa uliingia hapa ukapewa mafunzo na ukaelewa kazi ya Spika. Ndio maana nikifinya hapa unaniambia kwamba niendelee kuongea, kwa sababu unaelewa.

Ndio maana nikasema kuwa huyu waziri kwa kweli si daktari. Daktari akimwambia kuwa amedunga mtu, atajuaje kuwa amemdunga? Atajua namna gani ilhali hata hajui? Isipokuwa yeye adungwe, hajui kudunga? Ndio sababu nasema shida hiyo ndiyo tuliyo nayo. Huyu waziri pengine hata hajui watu hawana dawa kwa sababu pengine hata hajui kuangalia kama kuna dawa. Hata kama kuna makosa kwa wale madaktari ambao hawapeani dawa, angestahili kuwa mstari wa kwanza kuuliza dawa ziko wapi? Ni nani ana dawa? Hii kazi inafanywa vipi?

Nakumbuka wakati tulipoingia kwenye hili Bunge huyo waziri aliletwa akiwa Waziri wa Utawala iwapo nakumbuka vyema. Sisi, kwa hekima na ujuzi wa hili Bunge, tukaona huyu mtu hafai na kumtupilia mbali. Gavana wetu naye akaendelea mbele na kumpa kazi niliyosikia ni ya kupanga viti na kuangalia wakubwa. Nilipouliza zaidi niliambiwa inaitwa *protocol.* Kwa hivyo akaja akiwa *protocol,* kisha baadaye katika hiyo *protocol* sijui alipanga mambo gani vizuri kisha tukaona ameletwa akiwa waziri...

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Kagondu kwamba *protocol* ni *itifaki*. Kwa hivyo atumie *itifaki* ili iweze kueleweka.

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, unajua Kiswahili wakati mwingine ni ngumu. Bora tu Wajumbe niliokuwa nawaeleza kabla aje wamejua nilivyokuwa nikisema. Simlaumu kwa sababu hayo ni mambo yake na atajipanga, na asipojipanga atapangwa, na sisi huwa hatupangwi, asante. Katika hayo mambo ya afya naona kuna shida kwa sababu hospitali zetu haziendi vizuri na wananchi wetu wanaumia, watu wanakufa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Juzi kuna kijana mmoja aliyepata ajali ya pikipiki na akafa hapo. Niliposikiliza watu waliofika hapo walisema ya kwamba huyo kijana alifika hospitalini lakini badala ya kuhudumiwa, wale madaktari; sijui kama ni madaktari waliohitimu ama ni nguo tu walikuwa wamevaa, hawakuweza kumuangalia na kumtibu. Walimwacha tu hadi akafariki akiwa hapo. Si mara ya kwanza, ni mara nyingi tumesikia watu wanakufa kwenye hii hospitali yetu kuu.

Kama tungeruhusiwa na sheria wakati Gavana akiongea, ningemueleza kinagaubaga akiwa hapo ya kwamba hospitali zetu zimebadilika. Badala ya kuwa hospitali za kutibu zimekuwa hospitali za kuua. Ningemueleza hivyo na angejua, lakini sheria haituruhusu kuongea. Nasema hivyo na kuongea bila kujificha ili apelekewe HANSARD asikie vile ambavyo nimesema. Hizo hospitali ni mbaya na zimekuwa vyumba vya kuhifadhia maiti badala ya hospitali za kutibu watu wetu.

Bwana Spika, nikigeukia mambo ya barabara, naona kuwa barabara zimetengenezwa kutoka Novemba 4, 2019 hadi Januari 31, 2022, a *total of 1784km have been graded, then 677.49km have been gravelled respectively*. Hio inamaanisha ya kwamba tumetengeneza na kufungua barabara, na bado tunaendelea, lakini nikiwa hapo ni vizuri niseme ya kwamba katika Laikipia hakuna mtu mkubwa kuliko mwingine. Sisi sote tunastahili kupewa huduma kwa usawa.

Ni kama nilivyosema kuwa hili Bunge limekuwa la watu wachache wanaoketi chini na kusema jinsi wanavyolipwa na wengine kutolipwa, na watakavyotajirika. Jinsi watakavyolipwa pesa waende kwenye kampeni kana kwamba wengine wataletewa viti vyao kwa mikono. Hapa pia kuna sehemu nyingine ambapo kilomita nyingi za barabara zinajengwa kuliko nyingine. Sisi sote ni Wanalaikipia. Sote tunahitaji kupewa kwa usawa.

Tukienda Tigithi, wapewe haki na wapewe barabara, tukiingia Thingithu tupewe barabara kwenye sehemu zote. Kama wamepata kilomita 60, hata kama sisi watu wa Thingithu tunaonekana hatuna maana, tupewe angalau arobaini. Tunasikia wengine wanapewa sabini na wengine ishirini ama kumi na kitu. Hayo ni madharau na sioni tukienda vizuri. Juzi tuliambiwa ya kwamba wadi moja kwenye eneo moja wamefanya zaidi ya kilomita 100. Nikienda Tigithi najua kuna maeneo manne au tano lakini kuna eneo utapata hakuna hata kilomita moja. Hiyo si haki.

Bwana Spika, tunasema ni usalama. Ndiyo, ni usalama, tunahitaji Laikipia ilindwe lakini hata sisi tukiwa Thingithu tunahitaji usalama. Tukitembea kwenye barabara za Majengo *tunapigwa ngeta*, kwa hivyo hatuna usalama kwa sababu hatuna barabara. Kama ni usalama, tupeleke kila mahali. Ng'ombe zinaibwa Tigithi na kupitishwa kwenye kichaka na Segera kupelekwa kule kwingine. Huko hata hakuna barabara ilhali wanaihitaji.

Naonelea tuketi chini na kuongea kuhusu mambo ya barabara isiwe kwamba kuna wanaopendelewa na wengine hawafanyiwi. Mfano mzuri ni wadi ya Rumuruti ambapo mashine zimeingia juzi, wao pia wameumia. Hata kama wako upande wa rukwama na wanaendesha rukwama, wapewe haki. Hata kama wewe uko kwenye Azimio, sisi tulio kwenye rukwama tupatiwe...

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, ningeomba mwongozo wako kwa sababu swala tunalolijadili ni hotuba ya Gavana lakini nimesikia maneno mengine yameanza kuchomekwa chomekwa huko ambayo siyaelewi. Kwamba eti kuna watu wanasukuma rukwama, sijui namna gani, sielewi. Ni vizuri tuangazie sana hotuba yenyewe, naomba.

Speaker: Mheshimiwa Ndiritu, fafanua iwapo mnamwaga *murram* na rukwama ama mnafanya nini.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, asante kwa kumuelekeza Mheshimiwa Mutahi. Ukienda kwenye wadi yetu na wadi ya Rumuruti utapata kwamba barabara zinatengenezwa na rukwama. Kwenye katikati ya mji ni rukwama zinabeba na kutengeneza sijui koroga au nini, lakini ukija kwenye wadi nyingine unapata ni matrekta. Baadhi yetu tunaumizwa. Juzi sisi tumemwaga *murram* na rukwama hapa kwenye soko, hatuna hata lori. Ndio namaanisha kuwa hata kama wengine wanamwagiwa na rukwama, tuheshimiwe. Hiyo ni haki yetu.

La mwisho ni kuhusu maji, kwa sababu naona hotuba ya Gavana imegusia mambo yote. Maji ni muhimu na sote tunahitaji kupata maji kwenye Kaunti yetu. Mimi nikiongea hapa kuhusu watu wa Thingithu naelewa hata sehemu zingine za Laikipia wana shida. Wanasema kuwa Thingithu ina maji kwa asilimia tisini na kitu ilhali kwenye hiyo wadi utapata sehemu zingine kama za Njoguini, Burugutia na Sweetwaters hazina maji. Wako na shida. Hata kama tuna maji, ni ya kisima ambayo hata kupata ni shida.

Ningetaka pia, katika haya mambo ya miradi ya maji, nimeona wamepeleka maji Ngarendare kwenye wadi ya Mukogodo Mashariki. Hilo ni jambo la busara kwa sababu wananchi wa sehemu hiyo hawakuwa na maji. Ningeomba hio maji kuendelea na kufika hadi Mukogodo West na Kimanju, wapate maji inayotoka kwenye Mlima Kenya moja kwa moja wanywe badala ya kuchota kwenye mchanga. Tuko na shida ya maji na ningeomba hiyo sekta ya maji iangaliwe vizuri ili wananchi wa Laikipia wapate maji kwa njia rahisi.

Kuhusu biashara, tunaona ya kwamba biashara inaendelea vizuri katika Laikipia lakini nilivyosema hapo mbeleni, wananchi wanaumizwa na malipo ya leseni. Nimeona kuna pesa za mpango wa ukuzaji wa biashara. Huo mpango ni mzuri na tunaupenda lakini una kasoro. Tunaposema tunataka kuinua watu wa biashara, tusiegemee tu matajiri, walio na maduka na wenye viwanda. Tujue ya kwamba kuna wananchi wanaouza mboga, wengine wanauza nguo, wengine biashara zao ni ndogo sana na wengine ni wakulima.

Katika hiyo pesa, tungetaka kuona na kujua ya kwamba mwananchi anayeuza mboga pale kwenye soko ya kale ya Nanyuki, yule mchuuzi anayebeba vitu zake kwenye mkono, tunataka yeye pia apate pesa. Hatutaki iwe kwamba lazima uje na leseni. Ukimwambia mama mboga aje na leseni, ataitoa wapi ilhali yeye hupewa kadi ya shilingi ishirini ya kulipia leseni?

Nilipokuwa mwenyekiti wa idara ya biashara nilipendekeza kuwa mtu akilipwa leo na ana kadi, alipishwe tena kesho, na juzi amelipishwa, mtu aweke hizo kadi zote vizuri ili akienda kwenye benki aweze kupata pesa. Haijakuwa hivyo. Ukienda kwenye hizi pesa wanazosema ni za kuinua biashara zilizo kwenye benki za Co-operative, Equity na KCB pamoja na wengine walio marafiki wa serikali wanaopewa hizo kandarasi; mwananchi anayefanya kazi pale sokoni anakosa kupata hiyo pesa kwa sababu akiingia pale anakuta watu waliovaa suti kama mimi, watu ambao akiwaangalia hivi anashtuka. Wakimwona wanamuuliza anafanya nini pale. Anaonekana kama mtu asiyestahili kuwa pale ilhali serikali yenyewe ndiyo imempeleka pale.

Watu wanaouza mboga pale ninapowakilisha ama nguo za mtumba hawaendi hata kwenye benki kwa sababu hawana pesa za kuingia kwenye benki, wanaweka pesa zao kwenye Mpesa, mfukoni ama kununua mkebe na kuiweka humo ili waitoe baadaye kwa sababu hawajaendelea kiasi cha kuweka pesa kwenye benki. Ningeomba tuweze kuangalia kila mtu na kila sehemu ili mambo yote yaendelee vizuri.

Nikimaliza, nitasema kuhusu hii pesa bilioni moja nukta sita ya *Infrastructural Bond* tuliyopitisha kwenye hili Bunge. Tunaingoja kwa hamu maendeleo yaweze kufika mashinani na iweze kufanya kazi jinsi inavyostahili. Tunaomba kwamba itakapofika, sehemu ambazo hazijapata maendeleo vizuri zipewe nafasi ili kazi iendelee. Kwenye wodi ya Thingithu kuna barabara zitakazojengwa kwenye upande wa Bemwaki na Mahakama, kuna soko ambazo

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

zitajengwa, nasikia Matanya itajengwa, Mwireri pia na Kalalu pamoja na sehemu zile zingine ambapo wananchi wa Laikipia wako.

Namaliza na kushukuru nikisema kuwa tuwe kitu kimoja, tufanye kazi pamoja na sote tupendane kwenye hili Bunge. Isiwe kwamba kuna wala nyama na wala nyasi. Sote tuko sawa na ni Wajumbe na tunahitaji heshima. Ahsante.

Hon. Catherine Nyawira: Thank you, Hon. Speaker for giving me this chance to contribute to the Governor's speech. One is to echo the words of the previous speaker, Hon. Ndiritu who has spoken about fairness, openness and budgetary allocation in this Assembly, and discussing issues and putting them on the table. With all due respect, I think that is important. It is unfortunate when we have hearsay in this House and I believe those are the things that cause division and people behind the tent, which is unfortunate. With that in mind, I request that with your able leadership, you convene a meeting to discuss the budgetary allocation for this Assembly for this session. Thank you.

Moving on to the Governor's speech, one, I want to applaud the revenue collection by the Executive. The reason I do this is because, the key role that is able to run a government and do projects is revenue collection. However, the greatest question I would be asking is; have we ensured that Wanjiku is happy to pay these taxes? Have we ensured that the services sought are always given to them when they pay their taxes? Do they pay it happily? Are they able to make ends meet? For me personally, that is a question posed to this Assembly and myself. Have I done my oversight role to be able to know where this money goes, how it is utilized and, basically, is Wanjiku happy?

Hon. Speaker, on the issue of tax collection again, when we visit some wards on our oversight, I realize that some wards have benefitted more than others. I am not afraid to say this for fear of contradiction because the road network in some wards has a heavier presence than others. Why is that? In the initial plan for the leasing program, was it that Members did not sit down and come up with a proper program to ensure equity as opposed to quantity is put in place?

When I see us complaining, I feel very bad because it was our role. Either it was looked down upon or somebody just chose not to implement it. I remember when I came to this Assembly there was a project that was done of 15 km or 10 km, there was that initial project. That 10 km was never done in some wards, and in fact leasing came and did it. Because of the failure of oversight we do not have a report in place to make sure that such things are accounted for.

On the issue of the Infrastructure Bond on page three, we have borrowed in an election year. The results of that are that our taxes and revenue collection, the taxes that the business community pays will go higher. It is not without knowledge that we did this. We did this with full knowledge that someone will suffer. It is an election year when investors pull away to observe the political temperatures, when businesses are slower, when more money is poured into the economy by us politicians. Therefore, there is no need to cry over spilt milk. Taxes must rise, business permits must go up because of the role that we played.

On the Economic Stimulus Programme that was meant to boost and revive businesses, I have not seen a quarterly report coming to the floor of this House with the relevant committee. Therefore, its success and failure cannot be mentioned by a phrase presented to us by the Governor. On the issue of the healthcare, I belong to that committee, I am the Vice Chair and we as a committee have spoken in this Assembly passionately about the healthcare of our people. We have fought for facility improvement fund in this. We have fought for budget by

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

bringing numerous reports. It is with much pride that I recognize that your office recognizes the Health Committee as the most active committee.

However, I wish to point out that as my predecessor was speaking, when we were fighting for these things, he was at the forefront of sabotaging them. It is unfortunate that now he sees what we were fighting for. Mr. Speaker, I am not happy with what is going on but I am happy that the Governor's Office has prioritized preventive health care as opposed to curative because that is the only way we can save costs. The reason we are rebranding is because preventive health has reached an upscale and less people get sick but we reported that during the COVID times.

Unfortunately, when COVID came, more ailments came. More advanced care of ICU was needed and therefore we see more people dying as opposed to treating because of the complications that this disease presents. Probably we should engage the beyond zero van to do more oversight and outreach and more medical that comes in the community. Mr. Speaker, as I dwell further into the health issues, the Health Committee passed a budget, the budget was rejected by this House when the bond was passing.

This Committee asked for the names of the beneficiaries of NHIF. To date I am happy to report that it is unfortunate that that report has not come before this House. We have reached a point where we need to summon the CECM and find out what is it with these names. Let us not forget that before the COVID times when the government engaged AMREF to M-JALI projects and list names of households who earn less than a dollar a day and get that information. When that information came, there was the COVID times when there was full distribution, this people would go to get food in their cars.

This means they were in that list to benefit from NHIF but they did not realize it will be used for other purposes. That list did not reflect the very poor in the society. Mr. Speaker, I feel that hospitals can do better. Money can be put where they are supposed to be for example drugs, support and other projects. There will be openness and oversight roles.

The other issue is when we visited the health centres and dispensaries we realized that these health centres do not receive capitation from NHIF. This is money that goes back to the health centres to be able to help them run but they do not receive them on a timely manner. Therefore, the residents who are supposed to benefit from the health centres and dispensaries end up going to the level 4 hospitals to get treatment therefore congesting it and straining its resources further.

Mr. Speaker, I know capitation is not an issue of the County Governments but NHIF, so some of these failures and shortcomings are as a result of the National Government by failing to remit this on time. Hon. Speaker and Hon. Members, we had a leasing programme that was passed in this House. However, that committee has never brought a report to show us how it works and what it does.

Apart from what we see from the Governor informing on how many kilometres it has done, 17 and 84 kms, we do not know its efficiency. We are told we see but we do not know its efficiency, effectiveness, sustainability in the wrong run and I think once again it is a failure of this Assembly through the committees.

However, Hon. Speaker, I will be running for MCA in Nyandarua and I am happy to report that those people see what leasing has done as opposed to us complaining. In fact, one of the residents in one of the meetings said that when they reach Laikipia they know because

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

they put their motorbikes on free because there are no more bumpy rides. Somebody sees for us what we can't quantify for ourselves.

Mine is to urge the committee which unfortunately I am in, to do the oversight role with more passion. On the issue of distribution of water, this has been a success programme. As I was coming to Nanyuki, I was lost and found myself in Tigithi. I can witness the farming that has changed livelihoods. The water has changed many lives and I believe they benefit. They make money and live better lives honestly.

Let us sometimes give credit where it is due. Unfortunately, we have to be aware of an upward tariff that will soon be coming to make sure that people pay more for water. I don't know when it is coming and I hope that this Assembly and the people of Laikipia can dig more boreholes and have their own water being sustainable, plant more trees, have more vegetation so that our water tables do not go down.

On the issue of innovation and enterprise, if you go to page 7 and look at the details of who has done what in the wards in the very last column, I noticed very sadly that Sosian has not benefitted. I believe a lot of the animals that go out as meat, should have left their leather and Sosian should have benefitted. Is it that nobody from Sosian is creative? Is it that capacity is not being taken there? Mukogodo West has one, Mukogodo East has four and Segera has one. I feel very bad when people from there do not benefit from manufacturing yet I know there is a lot of capacity.

The last time I went for such a show, there was wine being made from the cactus, an invasive species that is endangering the livelihood of their cattle. I am glad Nanyuki has 169 and Igwamiti has 68; the ward that I come from. Mr. Speaker, I have met numerous of those beneficiaries. I buy my facial products from one of the beneficiaries. I drink wine from one of the beneficiaries. Some of the brands that I buy in the supermarkets are from the enterprise funds.

Truth is that the future of this country is in manufacturing. We cannot continue to import things from China. We cannot continue to benefit other counties and countries at the expense of us. We must initiate and I like the Governor's passion and commitment to doing the same. Mr. Speaker, I see that the budgetary allocation for the SME stood at Kshs.7.5 Million for the financial year ended 30th June, 2022. When I went through the budget, we gave the Governor an blank cheque. The figures to me look very new to be there. I don't think I approved it.

Electricity is one of the challenges that these SMEs face but the Governor is putting more money into cautioning them on electricity yet Laikipia has much energy and sun. If you look at Laikipia North, why can't we have an investment on solar. Wouldn't it be more sustainable? On the issue of security in Olmoran, Githiga, Sosian and Rumuruti, I feel passionately being the Chair of Cohesion Committee is that the Governor's work, commitment and initiative to mobilise everybody to back up and ensure that our boarders are secure is beautiful. It is work well done.

I have never seen such leaders visit our county. I have never seen Hon. Natembeya, Hon. CS Matiangi and other great leaders come together and speak as one for all reasons. For me that was passionate and great about the Governor. He literally moved his office to Nanyuki. He mobilised all the equipment to go and open up those roads because one of the challenges we face and why the bandits attack us is because of our road network.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Those people take advantage such that when we want to give help we cannot access them. I applaud the work that he has done and feel that a section of this statement is true and beautiful and Laikipia is beautiful. Thank you.

Hon. Joseph Suge: Thank you, Mr. Speaker…

Speaker: Did you second this motion yesterday or who seconded?

Hon. Joseph Suge: Asante, Mheshimiwa Spika kwa nafasi nyingine ambayo umenipatia ili niweze kutoa mchango wangu kulingana na hotuba ya Gavana wetu wa Laikipia, Mheshimiwa Ndiritu Muriithi. Mheshimiwa Spika, nilipopitia na kuangalia kwa ndani hotuba ya Gavana niliona maswala mengi ambayo yanahusu wanalaikipia, ameweza kuelezea Bunge hili tukufu. Mheshimiwa Spika, yale ambayo yaliniguza sana ni kwa ajili ya hatua ambayo Kaunti ya Laikipia imeweza kupiga.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) left the Chair]

[Temporary Speaker (Hon. Catherine Nyawira) took the Chair]

Kwa sababu wengi wamechangia kwanza kabisa ni kuhusiana na ushuru. Wakati mmoja nilisikia Mheshimiwa Mwai Kibaki aliyekuwa Rais na mkuu wa jeshi katika taifa letu la Kenya akisema ya kwamba kulipa ushuru ndio kujitegemea. Ukweli ni kwamba wanalaikipia wameweka kipao mbele kulipa ushuru ili Kaunti yetu iweze kuinuka na serikali iweze kupeana mahitaji na maswala ambayo yanahusu jamii ya Laikipia kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kulingana na hotuba nimeona ya kwamba ushuru wa Laikipia umeweza kuinuka. Mpaka kwa sasa tumefikia bilioni moja. Hii ni hatua kubwa na hongera kwa Wizara ambayo inahusika na ukusanyaji wa ushuru. Mheshimiwa Spika, pia tushukuru wafanyi biashara na wenyeji wa Laikipia kwa kuweza kulipa ushuru kwa wakati ambao unafaa. Langu ni kwamba inastahili kuwahimiza zaidi waweze kufikiwa kuhamasishwa umuhimu wa kulipa ushuru wakati ambao unafaa na vilevile kuangalia kulingana na matatizo ambayo yanakumba wafanyibiashara.

Biashara zingine ziko chini na zinastahili kuinuliwa juu. Zingine kwa sababu ya ushuru uko juu biashara zinaweza kuanguka. Kwa hivyo ni vizuri liweze kuangaliwa. Lingine ni kuhusiana na sekta ya afya. Nimeona juzi Gavana amezunguka Kaunti nzima akiongea na wananchi akipeana hoja zao kuhusiana na sekta ya afya na tunashukuru. Niliweza kutembelea hospitali ya Nanyuki na zahanati zingine mashinani. Nilikuta zote zimepigwa rangi lakini changamoto kubwa ni madawa. Ningeomba hili liweze kuangaliwa. Kuwe na madawa ili watu waweze kupata matibabu wakati wote wanahitaji.

Mambo ya MRI nimeona Gavana akisema ya kwamba itaanzishwa katika Hospitali ya Nanyuki. Pia ningesema hospitali ya Nyahururu iweze kuwa na kifaa cha kuweza kufanya MRI na CT Scan. Ni changamoto kubwa kwa sababu katika Magharibi mwa Laikipia watu wengi wanatumwa Nakuru na Nyeri. Juzi Serikali ya Kaunti ya Nyandarua wameweka CT Scan katika Hospitali ya Olkalou. Hilo limepatia hao watu afueni. Ningesema CT Scan iweze kuwekwa kwa Hospitali ya Nanyuki, Nyahururu, Doldol na Rumuruti ili watu wetu waweze kusaidika.

Swala lingine nyeti ni kuhusiana na maafisa ambao wanapeana matibabu. Najua kuna wauguzi, maafisa wa kliniki na madaktari ambao wamekuwa na changamoto na ni vizuri waweze kuongezwa ili kuwe na wataalam wengi ambao watasaidia watu wetu. Maswala ya matibabu yana gharama ya juu. Tukifanya hivyo watu wengi watakuwa wakipata matibabu kwa njia nzuri bila kutatizika na gharama ya juu kwa kwenda hospitali za kibinafsi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Swala ambalo linahusu barabara ni jambo ambalo limechangiwa na wengi. Ni vizuri Kaunti imekuja na mfumo mpya wa kuchukua mashine za barabara za kukodisha. Tumeona kazi ikifanywa katika pembe zote za Kaunti. Changamoto ambalo wengi wamesema ni kwamba aliye na macho haambiwi tazama. Kuna wadi zingine ambazo zimeweza kufaulu sana kupitia kukodisha mashine na wadi zingine zimeangamia kwa sababu wengi wamezingoja kwa zaidi ya miaka mitatu.

Nashukuru kwa sababu nilipoingia Mheshimiwa kutoka Thingithu alikuwa anahurumia watu wa Rumuruti na kusema ilibidi watu walazimike kutumia *wheelbarrow* kujenga barabara. Ningetaka kusema pia tulitumia trekta kuziba mashimo ambayo yalikuwa barabarani ilhali Wodi jirani Olmoran na Githiga wameweza barabara zaidi ya kilomita 150 kwa kila wadi na kuweka murram.

Kwa hivyo ni vizuri viongozi wa Kaunti waweze kuangalia usawa na uwazi katika utekelezaji wa kazi. Siyo jambo la maana na kawaida kiongozi ambaye analilia watu na kuona haki imetendekea, inapofika mahali kilio chake kinaisha ni pengine sikio halisikii kwa sababu mimi nitasema mbele ya kila mmoja kwamba ilibidi niweze kulalamika kwa kuandika barua ambayo iliweza kufika kwa ofisi ya Gavana.

Ndiposa mashine zimefika kwangu na nitasema jambo kama hilo halifai kufanyika tena katika serikali yeyote kwa sababu kila mmoja anahitaji haki yake na kila mtu analipa ushuru. Nawashukuru sana wenyeji wa Rumuruti kwa sababu kwa takriban miaka mitatu hawajaona mashine za kulima barabara lakini wamevumilia. Ingekuwa ni watu ambao hawakuwa na utu mwema kwangu mimi singeweza kupitia eneo za biashara katika mji wa Rumuruti. Ningekuwa narushiwa mawe na matusi.

Nashukuru Mungu kwa sababu walipata moyo wa uvumilivu. Walipata moyo kwamba kutakuja siku ambayo watafanyiwa. Nimalizie kwa kushukuru Gavana kwa sababu alipopata hayo malalamishi sasa tuko na mashine pale na tumeondoa *wheelbarrow* kwa barabara ili barabara zifanyike kwa mashine. Trekta zimerudi kwa mashamba kulima na kwa hivyo sasa tumeona kazi ikifanyika lakini changamoto ni kwamba kuwe na uwazi kila wakati na kusiwe na mapendeleo kwa sababu Wadi ya Rumuruti ndiyo ilikuwa ya mwisho katika sehemu za Magharibi mwa Laikipia ambayo iko na wadi sita. Wadi moja ambayo inawakilishwa na Mheshimiwa Suge, wa Rumuruti ndio ilikuwa ya mwisho. Nataka kusema mungu atusaidie sana na aturehemu kutokana na hii siasa tunaelekea.

Jambo lingine ni kuhusiana na maji. Tunaona miradi nyingi zimefanyika. Wakati huu ni msimu wa kiangazi. Katika hotuba ya Gavana alisema kuna haja ya kuweka pesa ndio kukidhi mahitaji ya wananchi wakati wa kiangazi. Ningesema mbali na kufikiria mambo ya chakula ni bora kuhakikisha ya kwamba maswala ya maji imepewa kipao mbele. Nimeona miradi mingi imefanyika kama ya ukulima na ni vizuri. Lakini kuna zile miradi za mabwawa na ziweze kukamilishwa. Mingi zimefanywa na zile zimebakia zikamilishwe ili wananchi waweze kupata maji. Vile vile vidimbwi ziwe mingi za kusaidia wakulima wakati wa kiangazi.

Kulingana na pesa za kuinua wanabiashara -*Enterprise Fund*, ni ukweli kuna biashara nyingi ambazo zimesaidika. Wakati wa Korona nyingi ziliadhirika. Nashukuru mipangilio ya Kaunti kuona ya kwamba hawa wanabiashara wameinuliwa kidogo ndio waweze kuendelea na biashara zao kama kawaida.

Swala hili tunapofikiria jinsi ya kukuza Laikipia kimaendeleo ningewasihi Wajumbe wa Bunge hili tufikirie kuinua Laikipia pia tunainua katika elimu. Nilipigwa na butwa na kushangaa sana kwa sababu ya kupitisha bajeti bila kuweka hela kidogo ya wanafunzi wetu ambao wanasoma. Tuko na wanafunzi ambao wanatoka familia za chini. Tunapofikiria

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

biashara tufikirie pia elimu ndio Laikipia ipate nguvu ya wakati huu na siku zijazo. Bajeti inakuja na ningeomba viongozi waweze kuweka kipao mbele na kuwe na hela kidogo za kuinua mambo ya elimu hasa upande wa ufadhili wa karo.

Kwa hayo machache, najua mengi yamesemwa kuhusiana na hotuba ya Gavana. Ni ripoti nzuri na kila kitu kimewekwa kwa sababu ni yale ambayo yamefanyika na yale yanayoangaziwa kufanywa. Mungu atusaidie kwa hiki kipindi kimebakia. Najua tunaelekea siasa tuwe tumefanya yale mambo Mungu atakuwa ametuwezesha kufanya na ndio Mwanalaikipia aweze kusaidika. Kwa hayo machache nashukuru.

Hon. Veronica Ikunyua: Asante sana, Bi. Spika kwa kunipa hii nafasi ndio nichangie hii hotuba ya Gavana. Kwanza, ningependa kupea Gavana changamoto kwa hii hotuba yake. Naona ameweza kutuweka kwa ukurasa wa kwanza. Ukienda kwa miladi hakuna mahali sisi tunaonekana. Ukiingia kwa hii bunge tuko na ripoti nyingi sana za mahali kote tumetembea. Hospitali, miladi, wawekezaji na wanabiashara na ningeonelea kwa sababu hii miladi yote imefanywa hapa imefanywa na gavana na wajumbe. Angeweka hapa ndio tuonekane siku moja pia tulikuwa tunachangia katika maendeleo ya Laikipia. Naona haoni Waheshimiwa kama wamechangia katika miradi.

Hii hotuba inamaanisha mambo mengi sana kwa wananchi. Wanaona wale wamefanya kazi, kama Bi. Gavana yuko hapo lakini hawaoni Waheshimiwa kama wamechangia. Kazi yao ni kukaa tu bunge. Wakati tunawekwa tukiangalia zile miradi itaonekana pia sisi tuko kazi.

Nikiingia upande wa Ushuru, naona tumeinuka. Wakaaji wa Laikipia wanalipa ushuru vizuri na ndio unaona miladi inafanyika katika Laikipia. Tukilipa ushuru Mheshimiwa Spika, tutaweza kutengeneza barabara zetu, kuweka maji, hospitali zetu zitaimarika, tutasaidia wanabiashara na pesa za kuwainua. Kama vile mnenaji mmoja alisema, kwamba tunahitaji kuangalia kama tukichukua ushuru wanabiashara wanachukulia lile jambo namna gani. Ni vizuri tuweze kusawazisha mambo. Tunahitaji kufuatilia kama wakitoa zile pesa zinawarudia vizuri? Zinaweka maji? Mabarabara? Ni vizuri tuangalie.

Mheshimiwa wa Mambo ya Hospitali zetu; Tuko na hospitali 84 za Kaunti na za wadi. Tujiulize maswali kama tunapatiana huduma ya afya bora ambayo ni ya kiwango cha juu. Ningependa kupea changamoto hospitali zetu kama Mwenyekiti wa kamati ya Afya. Naona wameanza LHS –Laikipia Health Service. Kama kamati, hawa mawaziri lazima wajue hawawezi fanya hii kazi bila kamati za Bunge. Kamati za Bunge ndizo zinakuja kuwatetea hapa. Ukiamua kufanya kazi bila kutujumuisha kama kamati ya Bunge kazi yako inainama.

Bi. Spika, nataka kusema ya kwamba tumeleta malalamishi hapa tukitaka kujua NHIF ni watu wangapi wameandikishwa. Tumeitisha hio ripoti karibu mwaka umeisha tukiitisha. Ripoti ya Kiandege hadi saizi bado. Nataka kusema, ukiangalia Rais wetu ameenda kufungua UHC. Mwanzo kabisa alihusisha kamati ya Afya ya Bunge kuu. Ndio tunaona Mheshimiwa Sabina Chege akienda mashinani kuelezea vile inasaidia.

Sisi tunajua vile UHC itasaidia na kuinua watu wetu. Watu wanagoneka saratani na malipo ya juu inakuwa kubwa kisha tunaitwa harambee. UHC zikiwa watu watakuwa wanaenda hospitali wanatibiwa bila malipo. Hilo ni jambo la maana na tunashukuru Rais wetu Uhuru Kenyatta. Ukiwa na NHIF na pia uko chini ya UHC hakuna kulipa hospitali. Ndio Gavana ameona itakuja kusaidia zile hospitali ambazo ziko na vifaa. Katika hotuba yake amesema tutawekewa ICU, MRI na zile vifaa ziwekwe kwa hospitali zetu za Kaunti na za wadi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mheshimiwa Spika, hayo yote yakifanyika itarudi ipitie Bunge. Itakuwa vibaya sana ikiletwa Bungeni na sisi wenyewe hatujafunzwa vile ile kazi itafanyika. Nasema kwamba wizara zote wajifunze kuhusisha kamati husika za Bunge.

Upande wa barabara, juzi walisema kuna hii ratiba ilipeanwa na naona wadi ya Nanyuki haiko hapa. Nafurahia nikisikia ilienda kutengeneza huko ndio wakati wa dharura kama usalama magari zetu za usalama zinatemea kila kona ya Laikipia yetu. Sio furaha yetu kusikia gari haikufika na watu walichomea manyumba. Hata hivyo tungependa kuwe na usawa kama kulivyokuwa mwaka wa 2017. Tulisikia Rumuruti walitengenezwa barabara kilomita 10 na kila wadi. Huu mpango wa juzi naona mimi sikupata wengine pia hatapata huu mpango wa mwisho ilhali pesa ililipwa. Haifai hata wadi moja ibaki bila kutengenezewa barabara katika mpango huu wa mwisho.

Kama kamati tuendelee kufanya kazi ya uangalizi ndio tuweze kujua kama ilisemekana Rumuruti haijawekwa, iliwekwa ngapi? Kama ni Nanyuki, Githiga na kwingine iliwekwa ngapi? Kusiwe na watu wengine wanakaribia Gavana sana wakiamka wanasema angalia huyo mtu wangu. Nasikia kuna mtu anajigamba hapa sana kwa kuwa karibu na Gavana. Ndiye anatengenezewa barabara na Gavana na wengine hawana. Sisi wote tuko hapa kwa sababu ya *wanjiku*. Tufanyiwe haki na kila wodi ifanyiwe haki.

Mheshimiwa Spika, hizi barabara zetu tulitengeneza hazina *drainage* mzuri kumaanisha hazina msingi wa kuishi miaka mingi. Unaweka leo mvua inanyesha na ile barabara inakatika. Tunatumai ya kwamba Gavana atafanya kazi na sisi na tufanye vizuri wakati tutaweza kuweka bajeti. Ningeomba tuweke bajeti ya kuhifadhi zile barabara zilitengenezwa 2017, 2018, 2019 na 2020 kwa bajeti ya ziada ndio turekebishe zile barabara ambazo zinaweza halibika. Marekebisho inaweza kuwa kidogo lakini mvua ikinyesha hizo barabara zinakuwa hazitumiki tena. Ningeomba katika hii bajeti ya ziada tuweke pesa ya kurekebisha na kuhifadhi zile barabara tulitengeneza.

Upande wa maji uko sawa. Maji ya NAWASCO inaenda hadi Kimanju. Maji ni uhai. Siku moja nilitembea upande wa Doldol na nikapata wakitumia maji ya mtaro, maji chafu. Sio furaha yetu kama Wabunge eneo moja inafurahia na ingine haifurahii. Kama vile Gavana na wajumbe wa eneo hilo wanasukuma maji safi ni furaha yetu. Hata hivyo ukienda kusukuma maji huko mbali, kumbuka hapa Nanyuki.

NAWASCO iko Nanyuki na ni huzuni kubwa sana kwamba eneo ya Ngando, Mukuri ambayo iko Nturukuma ambao wako sehemu ya wodi ya Nanyuki hawana maji. Ni huzuni kwa wakaaji wa eneo hilo. Wakiteremsha maji wakumbuke kushibisha wakaaji wa Nanyuki pia na maji safi ya mfereji.

Upande wa Mabwawa, tumezitengeneza na kuziweka nguvu za jua. Lakini ule mradi ni kama ulitengenezwa na watu waliokuwa na haja ya pesa. Ni vizuri tunapopatia mkandarasi kazi tuwe tunajua wametupatia hakikisho la utumizi wa muda gani. Sisi wanawake wa Meru tukilewa tuko hakikisho la kudumu ya miaka kumi. Ikiwa kama akina mama wako na hakikisho la miaka kumi inawezekanaje mtu aweke mradi wa kutumia nguvu za jua bila uhakika? Tungetaka kusema kwamba wizara ya maji ikiongozwa na Mheshimiwa Matunge ni vizuri wajue zile mabwawa zikiharibika zitatengenezwa aje na wanalaikipia watakuwa sawa bila shida ya maji.

Gavana sijaona akisema mambo ya nguvu ya umeme na mradi wa mataa mitaani. Tumeweka kwa bajeti ya 2020/2021na naona tuko na shida kubwa. Utapata mataa za mitaa zile zimechomeka unafuatilia hadi unachoka. Kama umeamua kufanya kazi nzuri fuatilia kila wizara. Kama hio wizara wameshindwa na kurekebisha zikichomeka warudishie ile jukumu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kwa wizara tawala. Hizo stima na mataa yanasaidia. Tunajaribu kuinua Laikipia iwe inafanya kazi kwa masaa 24. Hatuwezi fika hapo ikiwa zile mataa haijarekebishwa. Tunasema wizara zote zifanye kazi sawa sawa.

Tumeona SME wetu wamepewa pesa. Wadi ya Nanyuki wengi wameinuka washindi. Sio furaha yetu kuona wengine wamepata. Kama Igwamiti naona wamepata 68, nasema tupendane wote. Wengine wamepata moja. Sijui wanatumia mbinu gani ndio kupea wengine zaidi ya mia mbili, wengine mmoja na wawili. Ni vizuri watuelezee ni sheria gani walitumia ndio huyu apate na huyu asipate. Hawa wafanyakazi wote wameadhirika kwa pamoja.

Naona hili Bunge liko karibu kubakia mimi na wewe tuongee. Nataka kufungia hapo na niseme asante kwa hii ripoti kwa sababu imeweza kutufungua macho kuona ni wapi tunaweza rekebisha na ni wapi tutaongezea na ni wapi kumenya kazi na pia ni wapi hakujafanywa. Asante sana.

Temporary Speaker (Hon. Catherine Nyawira): Thank you Hon. Members. That ends the session on the deliberations on the Governor's Address.

ADJOURNMENT

Temporary Speaker (Hon. Catherine Nyawira): This House now stands adjourned until next week Tuesday, 15th February, 2021 at 2.30 pm.

The House rose at 10:27 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*